**BUNGE LA 13 | KIPINDI CHA 4**
**SENETI**

**KWA KANUNI YA MSWADA WA KATIBA YA KENYA (MAREKEBISHO), 2025 (MISWADA YA SENETI NAMBARI 13 YA 2025)**

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

**1. Madhumuni ya Mswada huu wa Katiba ya Kenya (Marekebisho), 2025 ni yapi?**

Mswada huu unalenga kurahisisha mfumo wa Bunge la Taifa na Seneti na kuimarisha ugatuzi. Unalenga kuoanisha majukumu ya kisheria ya Bunge la Taifa na Seneti kwa kurahisisha jukumu la utungaji wa sheria ili kuhakikisha kuwa kuna ushiriki wa kikamilifu katika mchakato wa kutunga sheria Bunge la Taifa na Seneti .

**2. Kwa nini kuimarisha ugatuzi ni kipaumbele katika Mswada huu?**

Ugatuzi ni kiini cha mfumo wa kikatiba wa Kenya kwa kuwa unapeleka huduma karibu na wananchi na kuendeleza usawa wa kimaendeleo. Hata hivyo, maoni yanayokinzana kuhusu majukumu kati ya Bunge la Taifa, Seneti, na Mabunge ya Kaunti yamedhoofisha utekelezaji wake kikamilifu. Mswada huu unalenga kushughulikia masuala hayo.

**3. Je, Wakenya watanufaika vipi kutokana na kuimarishwa kwa mfumo huu wa ugatuzi?**

Wakenya watanufaika kupitia uhakikisho wa mwendelezo wa huduma za serikali ya kaunti hata pale ambapo kunaweza kuwa na ucheleweshwaji wa kuidhinishwa kwa miswada inayohusiana na bajeti. Wakenya pia watanufaika kwa sababu kutakuwa na uwajibikaji na uangalizi ulioboreshwa kuhusu jinsi fedha zinavyotumika katika ngazi ya kaunti.

**4. Mswada unalenga kutatua changamoto zipi za kiutendaji katika ugatuzi?**

Mswada unashughulikia utata katika majukumu ya kutunga sheria ambao hapo awali ulisitisha au kubatilisha sheria. Zaidi ya hayo, Mswada unalenga kutoa ufafanuzi kuhusu jukumu la utungaji wa sheria katika ngazi ya kitaifa, ili kuhakikisha kuwa sheria zinazoidhinishwa katika ngazi ya kitaifa hazidhoofishi ugatuzi.

**5. Ni Ibara vipi mahususi za Katiba zinazorekebishwa au kubatilishwa?**

Mswada unapendekeza mabadiliko katika zaidi ya Ibara 20, zikiwemo 94, 95, 96, 108–116, 157, 173, 215, 221–224, 228–229, 233, 250–251. Hasa, unafutilia mbali Ibara 110 na 114.

**6. Mswada unaathiri vipi jukumu la Seneti?**

Seneti itapewa mamlaka ya—

- uhuru wa kutunga sheria, pamoja na kuwasilisha na kupitisha Miswada (isipokuwa ile inayohusu kukusanya mapato ya kitaifa);
- ushiriki katika michakato ya bajeti ili kuhakikisha kwamba wakati wa kugawa fedha, kaunti zinalindwa kwa kuhakikisha kuwa mapato yaliyokusanywa yanagawanywa kwa usawa na kwamba rasilimali zinaambatana na majukumu;
- utaratibu wa ukuu na uongozi kwa mujibu wa Ibara ya 108; na
- uwakilishi wa maslahi maalum na mashauriano kuhusu masuala yanayowahusu watu katika kaunti.

**7. Je, Bunge la Taifa litapoteza mamlaka yoyote kwenye Mswada huu?**

Hapana. Kwa hakika, Mswada huu unaweka wazi majukumu yanayoingiliana na kukuza ushirikiano kati Bunge la Taifa na Seneti.

**8. Ni nini kinachotokea katika upambanuzi wa "Miswada ya Fedha"?**

Mswada unafuta Ibara ya 114, inayofafanua "Miswada ya Fedha," kuondoa kutoeleweka kwa mara kwa mara kulikosababisha mgongano iwapo Mswada unahitaji maoni ya Seneti. Mabadiliko haya yanakusudia kupunguza ukwamishaji wa kisheria na kukuza ushirikishwaji katika kufanya maamuzi.

**9. Je, sasa Miswada inaweza kuanzishwa na Bunge la Taifa na pia Seneti?**

Ndio. Kwa mujibu wa mapendekezo ya marekebisho ya Ibara ya 109, Mswada wowote unaweza kuwasilishwa katika Bunge la Taifa au Seneti, isipokuwa Miswada ya kukusanya mapato ya kitaifa, ambayo inaweza kuanzishwa katika Bunge la Taifa.

**10. Miswada ya "ugavi" na ya "kuidhinisha matumizi ya fedha" ni nini, na inashughulikiwa vipi chini ya Mswada huu?**

- Miswada ya Ugavi (kama Mswada wa Ugavi Mapato ya Kaunti) sasa inaweza kuanzia Seneti, huku Bunge la Taifa likipendekeza marekebisho.
- Miswada ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha (matumizi ya serikali ya kitaifa) inaweza kuanzia katika Bunge la Taifa, huku Seneti likipendekeza marekebisho.
- Ikiwa Bunge moja halikubaliani na marekebisho ya lile lingine, theluthi mbili ya wabunge wengi kutoka kwa Bunge lililouanzisha mswada inaweza kutoyakubali.

**11. Je, mchakato wa usuluhishi unaathiriwa?**

Ndio. Ibara ya 113 iimefanyiwa marekebisho ili kuondoa Miswada ya Ugavi na Miswada ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha katika usuluhishi, hivyo kurahisisha kule kuzingatia na kupitisha

sheria zinazohusiana na bajeti, ikiwa ni pamoja na Taarifa ya Sera ya Bajeti, Sheria ya Kugawa Mapato, Sheria ya Ugavi wa Mapato ya Kaunti, Sheria za Kuidhinisha Matumizi ya Fedha, n.k.

**12. Je, Mswada huu unaunda ibara mpya ya kikatiba?**

Ndio. Mswada huu unaanzisha Ibara ya 199A, inayounda Hazina ya Bunge la Kaunti kwa kila kaunti, kusaidia gharama za utawala na uendeshaji wa mabunge ya kaunti.

**13. Kwa nini Hazina ya Bunge la Kaunti ilianzishwa?**

Ili kuhakikisha kwamba mabunge ya kaunti yanafanya kazi kwa uhuru na ufanisi, hasa katika kushughulikia uangalizi kwa serikali tekelezi za kaunti. Hii inafanya ufadhili wao kuwa rasmi na inakuza uhuru wa kifedha na uwajibikaji katika ngazi ya mashinani.

**14. Mswada huu unaathiri vipi mchakato wa bajeti katika ngazi za kitaifa na kaunti?**

Katika mswada huu—
- Makadirio ya bajeti yatakaguliwa na kuidhinishwa na Bunge la Taifa na Seneti;
- kamati za Bunge la Taifa na Seneti zitahusisha umma katika kuhakiki makadirio; na
- Bunge linaweza kuidhinisha utoaji wa muda wa fedha ili kuendeleza shughuli za kitaifa na za kaunti, endapo Bunge litachelewa kupitisha miswada ya ugavi wa mapato.

**15. Je, Mswada huu unakuza uratibu bora kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti?**

Ndio. Kwa kubainisha majukumu ya Bunge la Taifa na Seneti na kulainisha jinsi mapato na sheria zinavyosawazishwa, Mswada huu unakuza ushirikiano, unapunguza migongano ya kisheria kati ya Bunge la Taifa na Seneti, na unahakikisha utoaji wa huduma kwa Wakenya kwa wakati.

**16. Ni mabadiliko gani yanayofanywa katika uteuzi wa wanaoshikilia nyadhifa za ofisi za kikatiba?**

Mamlaka ya kuchunguza na kuidhinisha uteuzi wa wanaoshikilia nyadhifa za ofisi za kikatiba, (kwa mfano Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mdhibiti wa Bajeti, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, wenyekiti na makamishna wa tume za kikatiba), ambayo hapo awali yalikuwa ya Bunge la Taifa pekee, sasa yamekabidhiwa Seneti pia.

**17. Je, kutakuwa na ushirikishwaji wa umma kabla ya Mswada huu kupitishwa kuwa sheria?**

Ndio. Ibara ya 10 na ya 118 za Katiba zinawapa wananchi mamlaka ya kushirikishwa katika mchakato wa kutunga sheria. Kwa kuwa huu ni mchakato wa kurekebisha Katiba, unahitaji kura ya maoni ya kitaifa kwa mujibu wa Ibara ya 255. Hii inamaanisha kuwa maoni ya wananchi yatazingatiwa katika hatua mbalimbali: baada ya kuwasilishwa katika Bunge, wakati wa vikao vya kamati, na katika kura ya maoni yenyewe.

**18. Kwa nini ushirikishwaji wa umma ni muhimu katika kurekebisha Katiba?**

Katiba ndiyo sheria kuu ya nchi. Ushirikishwaji wa umma unahakikisha kuwa marekebisho yanawakilisha matakwa ya wananchi, yanalinda maslahi ya umma, na yanadumisha thamani za kidemokrasia. Kadhalika, unaimarisha uwazi na uaminifu katika maamuzi ya serikali.

**19. Je, Wakenya wanaweza vipi kuwa na uhakika kwamba maoni yao yatachukuliwa kwa uzito?**

Katiba inawajibisha Bunge kutafuta na kuzingatia maoni ya umma katika utungaji wa sheria (Ibara ya 118). Zaidi ya hayo, kamati za Bunge lazima ziandae ripoti zinazoonyesha jinsi mawasilisho ya umma yalivyopokewa na kuzingatiwa katika Mswada wa mwisho. Ripoti hizi zinakuwa sehemu ya kumbukumbu rasmi za kisheria.

**20. Je, kuna kinga za kisheria zinazohakikisha kuwa ushirikishwaji wa umma si jambo la kutimiza mahitaji ya sheria tu?**

Ndio. Mahakama zimeamua kuwa ushirikishwaji wa umma lazima uwe wa maana na si wa kijuujuu. Katika kesi kama vile *Hukumu ya BBI*, Mahakama zilisisitiza kwamba sheria yoyote itakayopitishwa bila ushiriki wa kutosha wa umma inaweza kutangazwa kuwa kinyume cha katiba na hivyo kuwa batili.

**21. Je, wananchi wanaweza kupinga mchakato huu wakihisi kupuuzwa?**

Ndio. Iwapo raia au kundi lolote litaamini kuwa mchakato wa ushiriki wa umma haukutosha au ulipuuzwa, basi linaweza kutafuta haki mahakamani kwa mujibu wa Ibara ya 22 na ya 258 za Katiba.

**22. Je, wananchi wanaweza kutoa maoni yao kuhusu Mswada huu kwa njia gani?**

Wakenya wanaweza kushiriki kwa —

- kuwasilisha hati za maandishi kwa Kamati za Bunge zinazohusika;
- kuhudhuria vikao vya hadhara au majukwaa ya wadau yanayoandaliwa na Bunge au serikali za kaunti;
- kujihusisha kupitia vyombo vya habari, mashirika ya kiraia, na mabaraza ya umma; na
- kupiga kura wakati wa kura ya maoni ya kitaifa, ambayo ni ya lazima kwa mabadiliko fulani ya kikatiba.

**23. Ni nini kitatokea kwa maoni yanayotolewa wakati wa mikutano ya hadhara?**

Mawasilisho ya kimazungumzo na ya kimaandishi yatakuwa —

- yanarekodiwa na kamati husika;
- yanahakikiwa pamoja na maoni ya wataalamu;
- yanaakisiwa katika ripoti ya kamati na marekebisho yanayoweza kufanywa katika mswada; na
- yanatolewa kwa umma iwapo yataombwa, hivyo kuongeza uwazi.

**24. Je, Wakenya wanaweza kufuatilia vipi ili kuona iwapo maoni yao yaliathiri Mswada?**

Unaweza—

- kusoma ripoti za kamati zitakazowasilishwa katika Bunge;
- kufuatilia mijadala ya pamoja ambapo wajumbe hurejelea mawasilisho ya umma;
- kupata muhtasari kutoka katika tovuti ya Bunge, mashirika ya kiraia, au vyombo vya habari; na
- kuhudhuria mikutano ya hadhara ya kujadili yaliyojiri baada ya vikao vya umma.

**25. Mswada huu utaanza kutumika lini ikiwa utapitishwa?**

Utaanza kutumika siku ya 14 baada ya kutangazwa rasmi kwa matokeo ya kura ya maoni ya kitaifa, kulingana na Ibara ya 255 ya Katiba.

**26. Kwa nini kura ya maoni inahitajika kwa ajili ya Mswada huu?**

Kwa mujibu wa Ibara ya 255(1) ya Katiba, marekebisho yoyote yanayogusia maeneo muhimu kama vile muundo wa ugatuzi, jukumu la Bunge, au uhuru wa tume za kikatiba na ofisi huru lazima yaidhinishwe na wananchi kupitia kwa kura ya maoni.

**27. Ni sehemu gani za Mswada zinazohitaji kura ya maoni?**

Marekebisho yoyote yanayopendekezwa na yanayoathiri muundo wa ugatuzi, majukumu ya Bunge, majukumu ya kaunti, au tume za kikatiba na ofisi huru lazima yapigiwe kura ya maoni, kama ilivyobainishwa katika Ibara ya 255(1) ya Katiba.

**28. Ni nani anayestahiki kupiga kura katika kura ya maoni?**

Mkenya yeyote aliyesajiliwa kama mpiga kura anastahiki kupiga kura katika kura ya maoni.

**29. Ni nani atakayeandaa kura ya maoni?**

Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) ina jukumu la kupanga na kuendesha kura ya maoni, kama inavyofanya katika uchaguzi mkuu.

**30. Ni nini kitatokea ikiwa umma utakataa marekebisho yaliyopendekezwa katika kura ya maoni?**

Iwapo wapiga kura wengi wataukataa Mswada huo wakati wa kura ya maoni, basi hautaanza kutumika na Katiba itasalia bila kubadilishwa. Bunge haliwezi kuenda kinyume cha matokeo ya kura ya maoni. Hii inasisitiza mamlaka makuu ya wananchi, ambayo ni kiini cha mageuzi ya kikatiba nchini Kenya.